JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA

ISO 9001:2015 Certified

*Mwanachama wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO), Codex Alimentarius Commission (WHO/FAO) na Wakala wa ISO na Mashirika ya Viwango ya Mataifa mbalimbali*

## MWALIKO WA KUSHIRIKI KATIKA JUKWAA LA BIASHARA LA VIWANGO (VIWANGO BUSINESS FORUM) TAREHE 5 JUNI, 2026 JIJINI DAR ES SALAAM

**Dar es Salaam, 21 Machi, 2026**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linaadhimisha miaka 50 tangu kuanzishwa kwake mwaka 1975. Katika kuadhimisha hatua hii muhimu, TBS imeandaa **Viwango Business Forum**, jukwaa maalum litakalowakutanisha wadau wa biashara na huduma kwa ajili ya kujadili kwa kina masuala mbalimbali yanayohusu nafasi ya viwango katika kukuza ushindani wa kibiashara na kuimarisha ubora wa bidhaa za Tanzania katika masoko ya ndani na ya kimataifa, kwa lengo la kuchangia maendeleo ya uchumi wa Taifa.

Kupitia jukwaa hili, wadau watapata fursa ya kubadilishana uzoefu na kujadili changamoto pamoja na fursa zinazohusiana na utekelezaji wa viwango katika biashara na uzalishaji. Jukwaa hili linatarajiwa kuwakutanisha viongozi na wawakilishi kutoka taasisi za Serikali, sekta binafsi, makampuni, wazalishaji, wafanyabiashara pamoja na wadau wengine wa maendeleo.

Jukwaa hili litafanyika tarehe 5 Juni 2026 katika Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam, kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana, ambapo Mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Balozi Wazir Salum.

Wadau wote wa biashara na huduma mnakaribishwa kushiriki katika jukwaa hili muhimu

Nafasi za ushiriki ni chache ambazo zitatolewa kwa watakaowahi kujisajili tu, hivyo mnashauriwa kujisajili mapema kwa kuscan msimbo wa QR ulioweka hapo chini.

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na **Bi. Deborah Haule** kwa namba **0713050805** au **Bw. Emanuel Bakashaya** kwa namba **0716957295.**

Imetolewa na;

**Scan kujisajili:**

Gladness H. Kaseka
**Meneja wa Uhusiano na Masoko**

*"Kuchochea Ubora na Usalama kwa Maisha Bora"*

**TBS MAKAO MAKUU**
Shirika la Viwango Tanzania
Barabara ya Sam Nujoma / Morogoro, Ubungo, Dar es Salaam
S. L. P. 9524
DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu Na: +255 22 245 0298/ +255 22 245 0206
Nukushi: +255 22 2450959
Namba ya Simu Bila Malipo: 0800110827
Barua pepe: info@tbs.go.tz
Tovuti: http://www.tbs.go.tz
Barua pepe kwa ajili ya malalamiko ya wateja: malalamiko@tbs.go.tz
Twitter: TBS_Tanzania
Instagram: tbs_Viwango

**TBS KANDA YA KATI**
Jengo la Kambarage
S. L. P. 2956
DODOMA, TANZANIA
Simu Na: +255 26 2520310

**TBS KANDA YA ZIWA**
Jengo la NSSF, Ghorofa ya 3
S. L. P. 1814
MWANZA, TANZANIA
Simu Na: +255 28 2505044

**TBS KANDA YA KASKAZINI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 2399
ARUSHA, TANZANIA
Simu Na: +255 27 2520143

**TBS KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI**
Jengo la NHIF, Ghorofa ya 7
S. L. P. 1674
MBEYA, TANZANIA
Simu Na: +255 25 2502848

**TBS KANDA YA KUSINI**
Jengo la MTUWASA
S. L. P. 1396
MTWARA, TANZANIA
Simu Na: +255 23 2334477

**TBS KANDA YA MAGHARIBI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 1276
KIGOMA, TANZANIA
Simu Na: +255 28 2804023